

Pg 25

Apigia debe mafuta, gesi

Na Lucy Ngowi

SERIKALI imeshauriwa kuweka mkazo zaidi kwenye suala la teknolojia kwenye viwanda vinavyohusiana na mafuta pamoja na gesi katika sera inayotungwa.

Aidha serikali imeshauriwa kuweka taasisi ambayo itatoa mwongozo katika eneo la kuzalisha maarifa na matumizi ya maarifa ya sekta ya mafuta ya gesi kama daraja la kuunganisha wadau wote katika kusambaza teknolojia hiyo nchini.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kisera kwenye mambo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STIPRO), Musambya Mutambala alisema hayo kwenye mjadala ulioandaliwa na Taasisi ya Policy Forum kwa kushirikiana na Haki Ardhi jijini Dar es Salaam uliohusu uwezo wa kiufundi wa ndani katika sekta ya mafuta na gesi.

Mutambala pia aliishauri serikali kuangalia bajeti yake ili itimize ahadi ya kuweka asilimia moja ya bajeti ya serikali kwenye mambo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Aliitaka serikali iangalie uwezekano wa kupanua wigo wa kupata msaada pamoja na sera itakayoweza kuelekeza kampuni za kigeni nchini zitoe asilimia moja ya mapato katika kusaidia taasisi ya utafiti nchini ili zitoe majibu ya uwezeshwaji wa teknolojia kwenye viwanda nchini.

Kwa upande wake aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Isidory Shirima alisema ni lazima nguvu kazi inayoajiriwa katika gesi na mafuta itoke ndani ya nchi lakini eneo hilo linahitaji utaalumu wa hali ya juu.

Naye Meneja Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini - Taasisi ya Kisera kuhusu utawala Bora katika tasnia ya uziduaji mafuta, madini na gesi Silas Olang alisema serikali ipo katika utaratibu wa kuandaa sera, sheria na kanuni ya kusimamia mafuta.

"Tunaelekea kuzuri kwa sababu ukiangalia hatua tunazochukua kwenda utawala bora katika kusi-mamia rasilimali hizi tayari tuna sera, sheria na sasa tunatengeneza kanuni. Nadhani tupo kwenye mkondo mzuri," alisema.